TANGAZO LA SERIKALI NA. 854 la tarehe 11/10/2024

SHERIA YA MIPANGO MIJI

(SURA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8 (1))*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA LUKUNGU YA MWAKA, 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga eneo la Lukungu ya mwaka, 2024.

Utangazaji wa Eneo la Upangaji Sura 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpango katika eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya jumla na ya kina katika eneo lililoainishwa kwenye Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri ya wilaya ya Busega.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la urasimishaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:-

“Unaanzia kwenye alama ya mpaka wa upimaji namba NP1 yenye majira - nukta 596476MS, 9757583KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa KS$208^{0}$3’17”MG kwa umbali wa kilomita 0.70 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba KGR1 yenye majira – nukta 596111MS, 9756898MG; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa KS$92^{0}$24’25”MS kwa umbali wa kilomita 1.60 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba KGR23 yenye majira – nukta 597669MS, 9756833MG; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa KS$134^{0}$35’46”MS kwa umbali wa kilomita 4.00 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MV637 yenye majira – nukta 600481MS, 9754060MG; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi kwa kufuata mto Lamadi hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba NP0 yenye majira – nukta 593546MS, 973767KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini

*Tangazo la Serikali Na. 854 (Linaendelea)*

- Mashariki kwa kufuata ziwa Victoria hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba NPO1 yenye majira – nukta 592541MS, 9757057KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi kwa kufuata mto Serengeti hadi ulipoanzia."

Dodoma,
2 Oktoba, 2024

DEOGRATIUS JOHN NDEJEMBI
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*